BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Pili – Tarehe 20 Septemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:
Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASUALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

53. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko ya waathirika wa udhalilishaji kwamba wanaripoti Polisi juu ya vitendo walivyofanyiwa kinyume na sheria na wamekuwa wakichukuliwa maelezo yao na baadae kutowasomea maelezo hayo hali ambayo inaleta mashaka kwa walalamikaji hao.

(a) Kwa kuwa utaratibu wa kusomewa maelezo yako ni jambo la kisheria, Wizara ina kauli gani kwa suala hili.

(b) Na kwa kuwa yapo madai kwamba maelezo yanayotolewa polisi hubadilishwa kabla kupelekwa mahakamani, Serikali haioni kwamba umefika wakati kwa mlalamikaji kupatiwa nakala “copy” ya maelezo yake baada ya kusomewa maelezo hayo na Polisi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

02. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hivi karibuni Baraza la Mji la Chake Chake limeanzisha utaratibu wa kutoza malipo ya shilingi 1,000/= kwa kila gari itakayoingia Chake Chake kutokea Wete au Mkoani.

(a) Ni mambo gani yamezingatiwa katika kuweka tozo kama hizo.

(b) Je, Baraza la Mji Chake Chake halioni linawaumiza wananchi kwa kuweka tozo hizo za rejareja hasa endapo dereva atatoka Mkoani atatakiwa alipe akifika Chake Chake, itakuwaje dereva huyo huyo akitakiwa alipe tena akiinga Wete na kurudi tena Chake Chake.

138. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Mkoa wa Mjini Magharibi ulifanya operesheni ya kukamata watu wanaofanya biashara ya ukahaba na mapenzi ya jinsia mmoja.

(a) Je, ni watu wangapi waliokamatwa na kufikishwa Mahakamani.

(b) Je, malengo hayo ya operesheni hiyo yamefanikiwa kwa kiasi gani.

(c) Je, kwanini zoezi hilo lilianza kwa kasi na sasa inaonekana kuzorota kinyume na malengo yake.

Wizara ya Biashara na Viwanda

70. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Mnamo tarehe 9/7/2018, Wizara ya Biashara na Viwanda imeripotiwa na vyombo vya habari ikieleza kuwa kuna mpango wa kuanzisha maeneo maalumu ya kujenga viwanda nchini ili kukuza uchumi wa nchi.

Je, ni maeneo gani ya nchi yetu ambayo yamechaguliwa kujengwa viwanda hivyo.

Wizara ya Elimu Na Mafunzo ya Amali:

38 MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli za binafsi, mara nyingi hutumia magari ya aina mbali mbali kwa ajili ya kuwasafirisha wanafunzi katika skuli zao. Lakini, kwa masikitiko makubwa, baadhi yao huchukuwa wanafunzi wengi na kusababisha msongomano wa wanafunzi katika gari hizo jambo ambalo ni hatari kwa wanafunzi hao.

Je, Wizara ina mpango gani wa kulinda usalama wa wanafunzi hao.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

44. MHESHIMIWA ASHA ABDALLA MUSSA (Jimbo la Kiwengwa) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Wizara ya Kilimo imetoa baadhi ya maeneo kumpa muwekezaji wa kiwanda cha sukari Mahonda kwa lengo la kulima miwa ili kuweza kuzalisha zaidi, miongoni mwa maeneo aliyopewa ni pamoja na Kilombero na Pangeni ambapo wananchi walikuwa wakilima mazao ya chakula, lakini mpaka leo hawajalipwa vipando vyao na mwekezaji huyo amekabidhiwa na ameanza kulifanyia kazi.

Je, ni lini wananchi hao watapatiwa haki zao.

Wizara ya Afya:

10 MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wataalamu wa “Radiography” ni muhimu katika Hospitali na vituo vingi vya afya. Hata hivyo, inaonekana wataalamu hao wapo wachache sana na wanahitajika katika kutoa huduma za “x-rays” na “ultra sound”. Ambapo katika Hospitali ya Mnazimmoja yupo mtaalamu mmoja tu ambaye anatakiwa afanyekazi na kusomesha wakati huo huo.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza wataalamu hao ili huduma hiyo ipatikane katika vituo vyetu vya afya.

(b) Kwanini Serikali haiwaajiri kwanza wataalamu kwa mkataba ili wawepo na kutoa huduma hospitalini na baadaye Serikali ikipata uwezo iwape ajira moja kwa moja.

(c) Je, Serikali inazo takwimu za mahitaji halisi ya wataalamu wa “radiography” katika Hospitali na vituo vya afya nchini.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

47. Mheshimiwa ALI KHAMIS BAKARI (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi jukumu la kuzima moto na kuokoa maisha na mali za watu. Hata hivyo, Kikosi hicho cha Uwanja wa Ndege kinakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa maji kwa ajili ya shughuli zake. Na kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar alitembelea eneo hilo na kuwataka wahusika wakuu kuweka miundombinu bora katika eneo hilo, na ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa.

(a) Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa.

(b) Je, hatuoni kufanya hivyo ni kurudisha nyuma juhudi za Serikali.

(c) Ni kiasi gani cha fedha kinahitajika kuondoa tatizo hilo.

39. MHESHEIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Safari baina ya Unguja na Pemba inayoanzia bandari ya Malindi hadi bandari ya Mkoani ni safari refu hasa pale bahari inapochafuka

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuanzisha Bandari ya Nungwi kwa safari za ndani baina ya Nungwi – Pemba kwa ajili ya kufupisha na kurahisisha safari baina ya visiwa vyetu hivi viwili.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti Bora ya Usimamizi wa Mahakama, Kufafanua Utumishi wa Mahakama, Kuanzisha Ofisi za Mtendaji Mkuu wa Mahakama na Mrajis, Kuanzisha Mfuko wa Mahakama, na Kuweka Masharti Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar, **(Raya Issa Msellem)**
20 Septemba, 2018. **KATIBU WA BARAZA.**